

LEARNING BY EAR 2011

“The Promised Land- A Story of African Migration to Europe”

EPISODE FOUR: “Lost in a Foreign Land”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann

KISUAHELI: Eric Ponda

List of characters by scene:

SCENE ONE: FARAHANI AND SULE IN A CYBER CAFÉ

- Farahani (m, 19)
- Sule (m, 19)
- Mohamed (m, 24)

SCENE TWO: LINDA IN TRANSIT AT A EUROPEAN AIRPORT

- Linda (f, 20)
- Info Lady (f, 30)

- **Man (m, age not important)**
- **Woman (f, age not important)**

SCENE THREE: FARAHANI AND SULE ON THE BEACH

- **Farahani (m, 19)**
- **Sule (m, 19)**

SCENE FOUR: LINDA AT THE SECURITY GATE IN TRANSIT

- **Linda (f, 20)**
- **Airport announcer (m/f, 35)**
- **Security officer (m, 40)**
- **Small crowd (3-4 ppl)**

INTRO:

Hujambo msikilizaji na kwa mara nyingine karibu katika mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Hii ni sehemu ya nne ya mchezo huu wa redio “**Ardhi ya Ahadi, hadithi kuhusu Wa-Afrika wanaohamia Ulaya**” kutafuta maisha bora. Katika kipindi kilichotangulia, Linda anawaaga familia, jamaa na marafiki kuelekea Ulaya kwa masomo zaidi. Akiwa kwenye ndege anakutana na Florence na mara moja wanaanza urafiki. Kwa upande mwingine huko Afrika Kaskazini, Farahani ambaye jaribio lake la kuhamia Ulaya kinyume na sheria linatibuka, na anakutana na rafiki yake Sule kwenye kibanda cha huduma za Intaneti. Hii ni baada ya Sule kuchelewa kupanda gari lililokuwa likiwasafirisha wahamiaji haramu barani Ulaya. Je nini yepi yatakayojiri katika kipindi cha leo? Endelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi “**Upweke katika Nchi ya Kigeni.**”. Lakini kwanza twende moja kwa moja

hadi kibanda cha simu kukutana na Sule na rafiki yake Farahani. Farahani bado anaendelea kuwasiliana kwa njia ya intaneti na rafiki yake Mohammed ambaye tayari amefaulu kufika Ulaya. Mohammed sasa ameanza mipango ya kutafuta hifadhi kama mkimbizi huko Ulaya.

SCENE ONE: FARAHAANI AND SULE IN A CYBER CAFE

1. SFX: BUSY CYBER CAFE ATMO

2. SULE: (impatient) Farahani! Unawasiliasna na nani kwenye mtandao? Nimekuwa nikikusubiri kwa zaidi ya saa moja sasa!

3. FARAHAANI: (excuses himself on the cyber chat) Subiri kidogo! Nipe sekunde moja Mohamed! (to Sule) Ni nini Sule? Huoni niko na shughuli nafanya? Nimekwambia subiri!

4. SULE: (sarcastic) Na nimekuwa nikikusubiri. Kisha kwa muda mrefu sana! Nani huyo unayewasiliana naye kwa mtandao? Mmmh? Mchumba wako?

5. FARAHAANI: Usilete ujinga wako! Ni rafiki yangu ndiyo! Tayari yeye amefanikiwa kufika Ulaya. Sasa anatafuta hifadhi ya mkimbizi. Ananielezea jinsi maisha yalivyombadilikia huko!

6. SULE: (curious) Maisha yake yamebadilika? Vipi? Kuwa mazuri au mabaya?

- 7. FARAHANI:** (**stressing**) Mazuri bila shaka! Nenda unisubiri sitakawia. Muda unakwenda ninavyozungumza na wewe! (**dismissive**) Ehee endelea! (**to speaker on chat**) Mohamed, samahani. Kwa hiyo unasema baada ya walinzi wa mpakani kukukamata kwenye mashua wakakusindikiza hadi kisiwani. Kisha baadaye?
- 8. MOHAMED:** (**on cyber chat**) Walitupa blanketi, na chakula, kisha wakamleta daktari kutufanyia uchunguzi wa kiafya, kwani baadhi yetu walikuwa wagonjwa na kupoteza maji mengi sana mwilini.
- 9. FARAHANI:** Kwa hivyo waliwaangalia vizuri?
- 10. MOHAMED:** (**uncertain**) Eee... ndiyo. Huku ni Ulaya bwana,... Unatarajia nini?
- 11. FARAHANI:** Sasa una habari kuhusu ni lini tena mashua hiyo itatia nanga au kuondoka bandarini?
- 12. MOHAMED:** Kwa hakika sijui! Lakini nitakutumia ujumbe pindi nitakapofahamishwa kuhusu habari hizo. Sasa naondoka kurudi chumbani mwangu.
- 13. FARAHANI:** Nasikia wivu,...hayo ndio maisha ninayoyatamani. Sawa asante Mohammed. Tutawasiliana. Kwaheri.

NARRATOR: Farahani ameanza kumuonea wivu rafiki yake anayeishi Ulaya ambaye bado anatafuta hifadhi ya ukimbizi. Je! Hifadhi hii ya ukimbizi ina maana gani. Endelea kuwa nasi ufahamu kitakachojiri. Kwa upande mwingine, ni alfajiri na mapema, na Linda anawasili katika uwanja mmoja wa ndege barani Ulaya, ambako ataabiri ndege nyingine kufika anakokwenda. Tusikie mambo yanavyomwendea.

SCENE TWO: LINDA IN TRANSIT IN A EUROPEAN AIRPORT

14. SFX: BUSY EUROPEAN AIRPORT ATMO

15. LINDA: **(completely lost in thought)** Oh, Mungu wangu! Huu uwanja wa ndege ni mkubwa, na una shughuli nyingi sana! Niko na muda wa dakika 40 kuabiri ndege nyingine. Hebu nimuulize huyu Bibi. **(to lady)** Samahani! Habari ya asubuhi, Je! Unajua kule....

16. WOMAN: Samahani niko na haraka, nakimbilia ndege yangu!

17. SFX: LUGGAGE BEING WHEELED AWAY BY PULLING

18. LINDA: **(shocked)** Siamini! Mbona hivi? Hata hangesubiri nimalize kuuliza! Hmm... labda nimuulize yule mwanamume aliyekaa pale akisoma gazeti **(to man)** Habari yako! Tafadhali unaweza kunielekeza Lango nambari.....

19. MAN: Sina habari. Ni mara yangu ya kwanza kufika hapa.

20. SFX: SHAKES NEWSPAPER

- 21. LINDA:** **(totally shocked)** Makaribisho moto moto haya! Hapa kila mmoja anafuata shughuli zake. **(realises)** Ahh! Ile pale meza ya maelezo, asante Mungu wangu! Habari? Tafadhali unaweza kunielekeza lango nambari tano?
- 22. INFO-LADY:** **(rapidly)** Msichana fuata hizi alama za kuwaelekeza wageni! Alama hizi zina maelezo kamili. Nenda moja kwa moja, pinda kulia, toka nje ya jengo, nenda moja kwa moja hadi kituo cha pili, kisha upande ngazi hadi ukumbi wa wageni wanaosubiri kuondoka. Lakini lazima upitie kwa vituo vya ukaguzi kuelekea lango nambari tano. Safiri salama!
- 23. LINDA:** **(confused)** Anasema nini? Kituo cha ukaguzi? Oh hapana! Na nimesalia na muda mchache sana... nilifikiri **(she starts to run)**
- 24. NARRATOR:** Linda anaanza kukimbia kuelekea sehemu alikoelekezwa, huku akiwa na wasi wasi sana. Majibu ya ukaidi aliyopokea kutoka kwa abiria wawili wa kwanza, kwa hakika yamemfanya kuwa muoga zaidi kwani siyo maisha aliyozoea nyumbani. Lakini hii ilikuwa kionjo tu kwa Linda. Wakati huo huo, Farahani amevumbua mbinu nyingine rahisi ya kumwezesha yeye na Sule kufika Ulaya. Na yuko tayari kumuelezea rafiki yake Sule mpango huu wanapotembea kuelekea ufuoni.

SCENE THREE: FARAHANI AND SULE ON THE BEACH

25. SFX: OCEAN ATMO

26. FARAHANI: (calmly) Sikiliza hapa Sule. Nafikiri ni vyema tuvuke upande mwingine wa bahari kwa kutumia mashua ya babako. Kwa kufanya hivyo hatutalazimika kuwalipa walanguzi. Unajua wanatoza ada kubwa sana.

27. SULE: (bursts out) Hahaha! (sarcastic) Hilo ni wazo zuri sana. Na ni vipi tutaweza kufanya hivyo? Wacha mzaha Farahani!

28. FARAHANI: Si utani! Mimi nafikiri wewe,... kama mtoto wa mvuvi unaelewa masuala haya ya mashua na bahari.

29. SULE: (confused) Si utani?...Nadhani umeanza mzaha.... Farahani! Kweli babangu ni mvuvi lakini hiyo haimaanishi chochote. Hatuwezi kusafiri kwa mashua hadi Ulaya, hatutafika!

30. FARAHANI: Wahamiaji wawili kwenye mashua ndogo wana nafasi nzuri ya kuingia Ulaya kuliko Mashua inayobeba kati ya wahamiaji 20 na 50.

31. SULE: Sahau, wewe unaota ! Unafikirii...

- 32. FARAHANI:** Ni kweli Sule! Tuna nafasi nzuri ambayo wengine hawana. Tujaribu!
- 33. SULE:** **(tempted)** Hmm... lakini.... Na je babangu? Familia yangu imetegemea uvuvi miaka nenda miaka rudi. Siwezi kuiba hiyo mashua moja. Ndiyo msingi wa maisha yetu. Anaweza kunilaani!
- 34. FARAHANI:** Nani anazungumza mambo ya kuiba mashua? **(cheeky laughter)** Wewe nenda umwambie kuhusu mpango wetu. Na hakika atafurahi kusikia hivyo na kutuazima mashua yake. Isitoshe kila mzazi angependa kusikia mwanae akiishi maisha mazuri. Na endapo tutafaulu ni familia yako itakayofaidika zaidi.
- 35. SULE:** Ndoto hii ya kwenda Ulaya imekufanya wazimu, Farahani! Lakini unamfahamu vizuri babangu ama wasema tu? Hapana siwezi! Ukitaka kuendelea na mipango yako basi nenda umueleze wewe mwenyewe!
- 36. FARAHANI:** **(annoyed)** Ah, Sule! Ni lini utakomaa wewe? Kila siku tunawaona mamia kwa maelfu wakipitia mji wetu kuelekea Ulaya. Kama wanaweza kufaulu kwanini sisi tusifanikiwe. Mbali na hayo tayari nimekwambia kwamba kuna watu watakaotusaidia pindi tutakapowasili Ulaya.

- 37. SULE:** Farahani, japo unajaribu kunishawishi, bado kuna maswali mengi sana. Mfano tukizama? Je tukishambuliwa na papa au tukisukumwa na mawimbi hadi sehemu nyingine tusiyotarajia? Na hizi ni changamoto tu za safari, bado hatujui yanayotusubiria Ulaya.
- 38. FARAHANI:** Sasa tatizo liko wapi iwapo tutaishia Ulaya au Marekani? Muhimu ni kuepukana na maisha haya ya umaskini yanayokumba bara letu!
- 39. SULE:** **(jokes)** Wewe unazungumza kama mwanasiasa, Farahani. Kwa hakika unafaa kuwa mwanasiasa!
- 40. FARAHANI:** Siwezi! Wanasiasa na viongozi wetu ndio wanaotusababishia mateso haya yote, wameharibu kabisa nchi yetu. Lengo lao ni kujaza matumbo yao tu huku wakiuza rasilimali zetu. Punde wanapoingia madarakani hawataki kung’atuka, na watatumia kila hila, kuwatesa na kuwakandamiza watu ili mradi tuwasalie madarakani!
- 41. SULE:** **(amazed)** Siamini waipenda nchi yako hivyo. Maana kila ukifungua kinywa chako ni Ulaya, Ulaya, Ulaya!
- 42. FARAHANI:** Ni kwasababu hakuna kitu kizuri kuhusu nchi yetu. Sikiliza, turejeele suala letu. Unapenda wazo langu?

- 43. SULE:** (thoughtful) Ni hatari sana Farahani! Lakini hakuna neno. Ni vyema pia kupitia changamoto kama hizi.
- 44. FARAHANI:** (pleased) Sawa kabisa! Sasa tunachohitaji kufanya ni kuzungumza na babako haraka iwezekanavyo.
- 45. NARRATOR:** Hatimaye Farahani amefaulu kumshawishi rafiki yake Sule kuhatarisha maisha yao kusafiria mashua ndogo ya babake Sule hadi. Je! Babake Sula atalipokeaje ombi hili? Wakati huo, Linda bado anahangaika kutafuta lango la kuondoka uwanja wa ndege. Amekwama kwenye mlolongo mrefu wa abiria wanaokaguliwa kabla ya kuondoka uwanjani. Na mara ghafla...

SCENE FOUR: LINDA AT THE SECURITY GATE, IN TRANSIT

46. SFX: AIRPORT ATMO

- 47. ANNOUNCER:** (via speakers) Bi Linda Maraga! Unaweza kuelekea lango nambari tano. Unachelewesha ndege. Tayari abiria wengine wameabiri ndege hiyo.
- 48. LINDA:** (panicking) Ni mimi! Ni mimi! Samahani,... samahani...nipisheni ? Ndege yangu inaondoka.. itaniacha!
- 49. SFX: GRUMBLING AND DISAPPROVING MURMURS FROM PASSENGERS**

50. SECURITY: Tafadhali toa mshipi wako, saa na chuma chochote. Hebu nione hati yako ya usafiri?

51. LINDA: Tafadhali nachelewa, ndege yangu inaniacha. Nimesikia jina langu kupitia kipaza sauti.

52. SECURITY: **(not bothered)** Umebeba Laptop, au mafuta yoyote kwenye mzigo wako? Je una kitu chochote cha kinachoweza kukata?

53. LINDA: **(aggravated)** Sina. Tafadhali nachelewa, nitaachwa na ndege yangu!

54. SECURITY: Kuwa mpole Dada. Sasa pitia kwenye mtambo ule wa ukaguzi.

55. SFX: BEEPING SOUND AS WHEN METAL DETECTOR DETECTS METAL

OUTRO:

Linda anapitia kwenye mtambo wa ukaguzi! Je atafaulu kuabiri ndege yake? Sikiliza sehemu ya tano ya mfululizo wa mchezo huu **Ardhi ya Ahadi – kuhusu Waafrika wanaohamia Ulaya.**” Je! Ni changamoto gani nyingine zinazomsubiri Linda anapojiunga na Chuo Kikuu Barani Ulaya? Je! Farahani na Sule nao watafanikiwa kumshawishi babake Sule kuwaazima mashua yao? Kwa haya na mengine mengi, ungana nasi kwenye sehemu ya tano. Pia ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa www.dw.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.